**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**


**SHULE YA SEKONDARI MASISIWE,**
**S. L. P. 147,**
**KILOLO – IRINGA**
**SIMU: - 0622858861**
**0766309482**


**18/12/2020**

**Majina ya mwanafunzi ___________________________________**
**S.L.P 2324**
**KILOLO - IRINGA**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASISIWE**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika **Shule ya Sekondari Masisiwe** mwaka **2021**, shule ipo kata ya masisiwe wilaya ya kilolo ipo umbali wa kilometa 57 toka kilolo, usafiri wa basi kutoka iringa mjini unapatikana kwa nauli ya shilingi 8000/= tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, hivyo unatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe **06/01/2021**. na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

## 2.0 SARE ZA SHULE

### 2.1 WAVULANA:

**(i)** **Suruali 2** rangi ya dark-blue mshono: suruali ya marinda **mawili (2**) chini iwe na upana wa 18 na mkunjo, mifuko miwili mbele na mmoja nyuma iwe na zipu, mkanda wa suruali upana inch 2 wenye lusi zingatia rangi ya (kitambaa darkblue namba moja).

**(ii)** Mashati mawili meupe(tetron) mikono mirefu.

**(iii)** Viatu vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi jozi **mbili (2).**

**(iv)** Sweta rangi ya darkblue lenye V upande wa mbele shingoni nalisiwe na maandishi au mochoro yoyote.

**(v)** Soksi nyeusi jozi **mbili(2).**

**(vi)** Mkanda mweusi usiwe na nembo yoyote

(vii)Sare za michezo:- bukta moja na fulana yake, raba na tracksuit rangi nyeusi zenye miraba myeupe.

**2.2 WASICHANA**

(i) **Sketi 2** ndefu zinazovuka magoti rangi ya dark-blue mshono wenye marinda nane (8) ya kupanga yenye mfuko upande wa kushoto, mkanda nchi 2

(ii) **Shati 2** nyeupe (tetron) mikono mirefu.

(iii) Viatu jozi **mbili (2)** vyeusi zenye kamba na visigino vifupi.

(iv) Soksi jozi **mbili (2**) rangi nyeupe

(v) Sweta rangi ya dark blue lenye (V) upande wa mbele lisilo na maandishi/mchoro.

(vi) Hijabu nyeupe kwa waislamu.

(vii) Sare za michezo:- bukta moja na fulana yake, raba na trucksuit rangi nyeusi zenye miraba myeupe.

**3.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

(i) Rimu **moja(1)** ya karatasi (**A4) moja**.

(ii) Faili la kati (la plastiki) moja la kutunzia mitihani aliyofanya pamoja na kumbukumbu nyingine.

(iii) Daftari kubwa 12 zenye kurasa 80 au kaunta kwaya 2 au kwaya 3

(iv) Kalamu 5 na penseli 5

(v) Mkebe 1 wa hesabu

(vi) Begi la kubebea

(vii) Rula

(viii) Kamusi 1 ya kiingereza (dictionary)

**4.0 MAHITAJI YA KIBINADAMU NA MAZINGIRA**

(i) **MATIBABU :** Mwanafunzi aje na kadi ya CHF (kadi ya bima ya afya kwaajiri ya matibabu atakapougua, ikumbukwe kuwa jukumu la matibabu ni la mzazi..

**(ii) VIFAA VYA CHAKULA.**

Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa vifaa/vyombo vya kulia chakula,ambavyo ni Sahani,Bakuli,Kikombe pamoja na kijiko.

**(iii) VIFAA VYA USAFI.**

Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na vifaa vya usafi kama vile; **NDOO (1) NDOGO, JEMBE (1) KWANJA (1). NB: VYOTE VIWE VIPYA.**

**KUKUBALI NAFASI ( Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi)**

Mimi (Mzazi/Mlezi)…………………………………………………………………………………

Nimesoma maagizo na taratibu/sheria za Shule na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia kwa umakini Mkubwa,na kuzielewa hivyo Ninakubali/sikubali mwanangu…………………………………………… Ajiunge na shule ya Sekondari ya Masisiwe na kwangu nitampa/sitampa vifaa na mahitaji yatakayohitajika kama ilivyoagizwa na uongozi wa shule.

Vile vile ninaahidi kuwa nitatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Walimu katika kumlea mtoto wangu kadri ya maadili ya mwanafunzi wa Kitanzania mpaka atakapo maliza kidato cha nne.

**ANUANI YA MZAZI/MLEZI**

**S.L.P………………………SIMU……………………….. SAINI……………………………….**

Iwapo mtoto atapatwa na tatizo kubwa la kiafya,ajali n.k basi mtu mwingine wa karibu wa kuwasiliana nae ni.

(1) Jina ……………………………………
Kijiji ………………………………….
Anuani yake ……………………………
Namba ya simu……………………………

(2) Jina …………………………………….
Kijiji ……………………………………...
Anuani yake ……………………………..
Namba ya simu …………………………….

NB: ***Kumbuka kufuta sehemu isiyohitajika.***

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY**

**MASISIWE SECONDARY SCHOOL**

**<u>MEDICAL EXAMINATION FORM</u>**

To be completed by a medical officer in respect all Form I entrants

Pupil's full name:……………………………………………………………………………

Age……………………….. Year…………………..Sex……………

Blood count (Red and White)………………………………………………………………

Stool examination…………………………………………………………………………….

Syphilis and other venereal diseases

test……………………………………………………………………………………………

T.B test………………………………………………………………………………………..

Eye test……………………………………………………………………………………….

Ears…………………………………………………………………………………………..

Abdomen…………………………………………………………….................................

Urine for plane test…………………………………………………………………………..

Test for pregnancy (for girls only)……………………………………………………….…

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g. physical defects impartment)

Infection chronic or family diseases etc.

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

……………

**I certify that the above is fit/unfit pursue his/her lesson/duties as required**.

Station…………………………Signature…………………………………………………

Date……………………………Designation………………………………………………

**Note: Medical Officer**

At the time of examination please treat the individual for any ailments you note, pupils/employee. This completed form should be sent to the school with you acceptance form brought when you come to school. No pupils any enrol or person any employment with certificate or physical fitness.

## 5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule ya Sekondari Masisiwe inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara Elimu Sayansi na Teknolojia,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:-

(a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
(d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wakati wopte na
(i) Kutunza mali za umma.

## 5.1 MAKOSA YAFUTAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji Bangi,Cocaine,Mirungi na kubeli.
(e) Kupigana au kupiga.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito/Kupata Mimba.
(i) Kuoa au Kuolewa.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kugoma,Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi.

**KARIBU SANA**

**………………………………**

**UPENDO I.KUNZUGALA**
**MKUU WA SHULE**

**SIMU: - 0622858861**
**0766309482**